JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 1575,
Iringa,
Simu : (026) 2700157
Nukushi : (026) 2703014
Baruapepe : rbciringa@pccb.go.tz
Mtandao : www.pccb.go.tz

IRINGA – MEI, 2023

WANANCHI IRINGA WANUFAIKA NA PROGRAMU YA TAKUKURU RAFIKI.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Iringa imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake katika robo ya Januari hadi Machi, 2023 ambapo mkazo uliwekwa katika kuzuia vitendo vya rushwa katika maeneo mbalimbali kwa kuhamasisha Wananchi kutambua wajibu wao wa kuzuia vitendo vya rushwa ambavyo ni kikwazo kwa Maendeleo ya Taifa.

Katika kipindi cha **Januari hadi Machi 2023** TAKUKURU Mkoa wa Iringa imepata mafanikio makubwa katika kutatua kero za wananchi katika maeneo yao kupitia Program ya **TAKUKURU RAFIKI** iliyoanza kutumika Mwezi Februari, 2023, ambapo Kata sita zimefikiwa katika Hamashauri za Manispaa ya Iringa (02), Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo (02) na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi (02).

1. UZUIAJI RUSHWA

TAKUKURU Mkoa wa Iringa imefuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo **10** yenye thamani ya Shilingi **Bilioni 7.3** katika sekta za Afya, Maji, Barabara na Fedha (mapato ya Halmashauri). Kati ya miradi hiyo, **miradi saba** ifuatayo ilionekana kuwa na mapungufu na hatua mbalimbali zilichukuliwa.

SN	JINA LA MRADI	YALIYOBAINIKA	HATUA ZILIZOCHUKULIWA
1.	**H/W Iringa** Ujenzi wa Mradi wa usambazaji maji Isupilo, Itengulinyi, Lumuli na Magunga wenye thamani ya TZS **2,060,155,965.00** Mradi huu unaendelea.	Mradi ulichelewa kidogo kwa Mkandarasi kukosa mabomba ya kumalizia eneo korofi (swampy area)	• TAKUKURU iliingilia kati kwa kukutana na Mkandarasi na kumhimiza kukamilisha mradi kwa wakati.
2.	Mradi wa ujenzi wa barabara ya Makuka hadi Migoli (15.63 km) wenye thamani ya	• Ucheleweshwaji wa kukamilishwa kwa mradi unaotokana na uzembe wa Mkandarasi	• TAKUKURU ilishauri Mkandarasi aandae Mpango Kazi mpya (Revised Working

	TZS. **376,914,000.00** (bila VAT)	kwa kuwa Mkataba unaonesha tarehe ya kuanza mradi ni **28.10.2022** na muda wa kumaliza ni tarehe **28.04.2023** • Mkandarasi hakuwepo kwenye eneo la mradi.	programme) utakaotekelezwa. • Ilishauriwa kifanyike kikao cha Wadau kati ya TAKUKURU, Mkandarasi na Mwajiri (TARURA Mkoa wa Iringa) pamoja na Meneja wa Mradi (TARURA Wilaya ya Iringa) kujadili changamoto na hatua za kuchukua.
3.	Ufuatiliaji wa matumizi ya mapato ya ndani ya **Halmashauri ya Wilaya ya Iringa** kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023(Julai 2022 hadi Disemba 2022), jumla ya kiasi cha Shilingi **328,567,782.63**	• Halmashauri imeshindwa kurejesha (failure to recover) fedha iliyokopeshwa kwa vikundi kwa wakati na wengine kushindwa kurejesha kabisa • Ukosefu wa mafunzo ya elimu ya biashara na masoko kwa vikundi. • Vikundi kutosimamia kilichopo katika andiko la mradi.	• Viongozi wa Serikali za Mitaa na Kata washirikiane na Maafisa maendeleo ya Jamii katika maeneo husika ili kuhimiza marejesho ya mikopo yafanyike kwa wakati. • Halmashauri kwa kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii wa wilaya na Kata waratibu na kutoa mafunzo kwa vikundi vyote vilivyokubaliwa kupata mkopo juu ya masuala ya uongozi, usimamizi wa fedha, uendeshaji wa miradi na utoaji wa taarifa hususan zinazohusu mkopo husika kama Kanuni za utoaji wa mikopo na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wananwake, vijana na watu wenye ulemavu za mwaka 2019 zinavyoelekeza. • Viongozi wa vikundi na Maafisa Maendeleo wahakikishe vikundi vinatekeleza miradi iliyoombewa fedha katika andiko la miradi.

4.	Ufuatiliaji wa matumizi ya mapato ya ndani ya **Halmashauri ya Manispaa ya Iringa** kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023(Julai 2022 hadi Disemba 2022), jumla ya kiasi cha Shilingi **410,785,840.00**	• Halmashauri ya Manispaa ya Iringa imeshindwa kurejesha (failure to recover) fedha iliyokopeshwa kwa vikundi kwa wakati au kushindwa kurejesha kabisa • Ukosefu wa mafunzo ya elimu ya biashara na masoko kwa vikundi vya Manispaa vilivyokopa. • Vikundi kutosimamia kilicho katika andiko la mradi na hivyo kukiuka taratibu za mikopo.	• Viongozi wa Serikali za Mitaa na Kata washirikiane na Maafisa maendeleo ya Jamii wa katika maeneo husika ili kuhimiza marejesho ya mikopo yafanyike kwa wakati. • Elimu kuhusu taratibu za mikopo itolewe kwa wahusika. • Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa waelimishe wanavikundi kuhusu umuhimu wa kufuata taratibu za mikopo.
5.	Utengenezaji wa barabara ya Makondeko-Ndolezi kwa kiwango cha lami inayogharimu kiasi cha TZS **333,509,000.00**	• Mkandarasi amekuwa nyuma ya muda hivyo kusababisha kuchelewa kwa mradi. • TAKUKURU imeingilia kati kwa kuitisha kikao na TARURA ili kupanga mikakati ya kuhakikisha mradi unakamilika kwa ubora na kwa wakati.	• Mradi upo katika hatua za awali na hatua za haraka zimechukuliwa ili kukamilisha mradi huo kwa wakati.
6.	Ufuatiliaji wa matumizi ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023(Julai 2022 hadi Disemba 2022), jumla ya kiasi cha Shilingi **1,400,000,000.00**	• Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi imeshindwa kurejesha (failure to recover) fedha iliyokopeshwa kwa vikundi kwa wakati au kushindwa kurejesha kabisa • Ukosefu wa mafunzo kwa wakopaji • Wakopaji wanatumia fedha	Ushauri umetolewa ili - Ufuatiliaji wa fedha zilizokopeshwa ufanyike ili kurejeshwa kwa wakati. - Elimu kuhusu taratibu za mikopo itolewe. - Maafisa maendeleo ya Jamii waelekeze wanavikundi kuhusu matumizi ya fedha wanazokopa kwa

		walizokopa kwa matumizi nje ya andiko.	kufuata andiko la mkopo
7.	**Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo** Ufuatiliaji wa matumizi ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023 (Julai 2022 hadi Disemba 2022), jumla ya kiasi cha Shilingi **124,930,000.00**	• Ukiukwaji wa taratibu za mikopo ikiwa ni pamoja na mikopo kutolewa kabla ya taratibu kukamilishwa • Mikopo kutorejeshwa kwa wakati • Mikopo kutumika kinyume na andiko lilivyoelekeza.	• Taratibu za mikopo zifuatwe na wanaokiuka wachukuliwe hatua za kisheria • Maafisa Maendeleo ya Jamii wafuatilie mikopo hii ili irejeshwe kwa wakati na kwa matumizi sahihi kulingana na andiko.

UCHAMBUZI WA MIFUMO NA UDHIBITI

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2023 zimefanyika **Chambuzi mbili (02)** za mifumo katika sekta za Misitu na Sekta Binafsi.

S.N	KAZI ILIYOFANYIKA	LENGO	YALIYOBAINIKA	MAKUBALIANO
1.	Uchambuzi wa mfumo katika uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu katika wilaya ya Iringa.	Kuchunguza hatari au mianya ya rushwa katika usimamizi wa mazao ya misitu wilaya ya Iringa.	• Usimamizi dhaifu katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na mazao ya misitu, katika mfumo wa ukusanyaji kodi na ushuru, ukokotoaji wa kodi na ushuru. • Usimamizi dhaifu wa uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu.	• Kusimamia na kutekeleza ipasavyo Sheria, Kanuni na Taratibu za usimamizi wa mazao ya misitu. • Kuandaa na kutekeleza Mikakati ya kuzuia rushwa katika mchakato wa uvunaji. • Kuimarisha

				usimamizi na ukaguzi katika maeneo ya uvunaji. • Kuongeza idadi ya Watumishi wa kada ya misitu ngazi ya Kata na wilaya.
2.	Uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa vikundi vya Kampuni ya Farm for the Future	Kufuatilia taratibu za utoaji fedha za wanachama wa kikundi cha Kampuni ya Farm for the Future kiasi cha TZS.12m zilifuatwa au kulikuwa na ukiukaji baada ya TAKUKURU kupokea malalamiko toka kwa Wanachama hao na TAKUKURU(W) ya Mufindi kubaini kuwa hakukuwa na jinai ila ni ukosefu wa elimu ya kutosha kwa wananchama.	Ilibainika Kampuni ya Farm for the Future haikutoa elimu ya kutosha kwa wanakikundi cha Local Farmers. Ilidaiwa baada ya kuwatafutia mkopo Sh. 12m toka kwa wadhamini wao walidhani kuwa fedha hiyo ni kwa ajili ya matumizi yao, kumbe walitakiwa kununua hisa za Kampuni hiyo ili waweze kunufaika baadaye.	Ilishauriwa Kampuni iwape elimu wanakikundi hao kuhusu utaratibu wa kufuata ili waweze kunufaika na uwekekzaji katika Kampuni.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA TAKUKURU RAFIKI

TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA TAKUKURU RAFIKI (TR) KWA KIPINDI CHA FEBRUARI NA MACHI 2023 NGAZI YA MKOA

Idadi ya kata zilizofikiwa	**Idadi ya kero zilizotolewa**	**Idadi ya kero zilizotatuliwa**	**Mifano ya kero kisekta na namna zilivyotatuliwa**	**Mafanikio ya TR katika mkoa**
06	**97**	Kero **74** zilipatiwa ufumbuzi baada kufanyika **vikao na Watoa huduma na Wanufaika kupewa mrejesho.**	• Ukosefu wa gari la takataka na Dampo la kutupia takataka. **(Afya)** **UTATUZI** **……** • Zahanati hazina dawa za kutosha na vifaa tiba **(Afya)** **UTATUZI** **……** • Kukosekana kwa mitandao ya maji taka **(Maji).** **UTATUZI** **……** • Bili za maji hazipatikani kwa wakati.**(Maji).** **UTATUZI** **……** • Barabara kutopitika majira ya mvua **(Barabara).** **UTATUZI** **……** • Mitaro ya maji kujaa wakati wa mvua na kumwaga maji kwenye nyumba za wakazi **(Barabara).** **UTATUZI** **……** • Hakuna usafiri wa Bajaji katika	• Utoaji wa huduma kwa Wananchi umeimarika. • Kuboreshwa kwa Usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo • Kuimarika kwa misingi ya utawala bora na kupungua kwa vitendo vya rushwa katika utoaji huduma. • Kuongezeka kwa wigo wa ushirikishwaji wa Wadau katika mapambano dhidi ya rushwa. • Ushiriki wa karibu wa wananchi katika mapambano dhidi ya Rushwa • Kupunguza kero kwa wananchi katika kupata huduma

			baadhi ya mitaa **(Usafirishaji)** **UTATUZI** **……** • Umeme kukatika mara kwa mara. **(Nishati)** **UTATUZI** **……** • Doria ya Polisi inafanyika mara chache sana katika mitaa (**Polisi)** **UTATUZI** **……** • Utaratibu wa kutambua wanufaika wa TASAF uangaliwe upya **(TASAF)** **UTATUZI** **……** • Kuhamisha fedha za mradi wa maji kupeleka kny ujenzi wa barabara bila taarifa kwa wananchi**(Maji)** **UTATUZI** **……** • Gharama za kujifungua kutokueleweka na hakuna stakabadhi **(Afya)** **UTATUZI** **……** • Kulipa fedha kwa ajili ya dhamana katika vituo vya Polisi **(Polisi)** **UTATUZI**	

			…… • Kutoweka mipaka ya maeneo ya serikali **(Ardhi)** **UTATUZI** …… • Oparesheni za usafi kutofanyika kwenye mabucha na vilabu **(Afya)** **UTATUZI** …… • Askari Polisi kuomba rushwa wananchi**. (Polisi)** **UTATUZI** …… • TARURA kutoshirikisha wananchi katika utekelezaji wa miradi yao **(Ujenzi)** **UTATUZI** ……	

2. UELIMISHAJI UMMA:

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2023 kazi za **Uelimishaji Umma** zimeendelea kuleta tija kwa kufanyika Uhamasishaji kwa Wananchi, Watumishi wa Umma, Asasi za Kiraia na Klabu za Wapinga Rushwa ili kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU kwa kuzingatia Kauli Mbiu ya ***"Kuzuia Rushwa ni Jukumu lako na Langu; Tutimize Wajibu wetu."*** Kazi zilizofanyika katika kipindi husikani kama zifuatazo:
Semina **46**, mikutano ya hadhara **22**, vipindi vya redio **04**, kuimarisha klabu za wapinga rushwa **46**, kuhudhuria Onesho **01** na uandishi wa habari/makala **04.**

3. KAZI ZA UCHUNGUZI

IDADI YA MALALAMIKO YALIYOPOKELEWA - 50			
Malalamiko		**Sekta**	**Hatua zilizochukuliwa na kufikiwa hadi sasa**
Rushwa	**35**	TAMISEMI (28) AZAKI (04)	Taarifa **35** zinazohusu rushwa zimeshughulikiwa kwa mujibu

		Mahakama (2) Kilimo (2) TANAPA (1) Ardhi (4) Polisi (2) Misitu (1) RITA (4) Magereza (1) TARURA (1)	wa sheria kwa kuanzisha Uchunguzi, ambapo zimefikia katika hatua mbalimbali za uchunguzi.
Yasiyo rushwa	**15**		Taarifa **15** zilizobaki ambazo hazikuhusu rushwa, zimeshughulikiwa kwa njia ya uelimishaji na ushauri.

MASHTAKA

Idadi ya kesi mpya zilizofunguliwa HAKUNA	**Idadi ya kesi zilizoamuliwa 01**	
Idadi ya kesi zinazoendelea mahakamani	**01**	
	zilizoshinda	**Zilizoshindwa**
	01	**HAKUNA**

4. USHIRIKIANO NA WADAU

S.N	MDAU	MAENEO YA USHIRIKIANO	MAFANIKIO YALIYOPATIKANA
1.	Wanaklabu za Wapinga rushwa na Vijana.	Kuhamasisha Jamii kushiriki mapambano dhidi ya rushwa kwa kuelimisha na kutoa taarifa za viashiria vya rushwa	Hamasa imeongezeka kwa Wanaklabu na Vijana kwa kushiriki katika matamasha yanayoandaliwa na TAKUKURU, kutoa elimu kwa Jamii, kutoa taarifa za viashiria vya rushwa na kusimamia miradi ya maendeleo.
2.	Wananchi	Kushiriki katika mikutano ya hadhara, semina, matamasha, kutoa taarifa za vitendo vya rushwa.	Hamasa imeongezeka kwa wananchi kushiriki katika mikutano ya hadhara, kutoa taarifa za viashiria vya rushwa na kusimamia miradi ya maendeleo.

3.	Mamlaka za Serikali za Mitaa	Semina kwa Watumishi wa Halmashauri, Katika kazi za ukaguzi wa miradi, katika kazi za udhibiti wa mifumo, kushirikiana kupata wataalamu wa kutoa ufafanuzi katika vipindi vya redio vinavyorushwa na TAKUKURU mf. TASAF	Mabadiliko chanya ya utendaji wa Watumishi katika utoaji wa huduma, ushirikiano unarahisisha kazi za TAKUKURU hasa katika ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo na udhibiti wa mianya ya rushwa katika mifumo.
4.	Vyombo vya Ulinzi na Usalama.	Kushirikiana katika utoaji elimu ya mapambano dhidi ya rushwa(Polisi, Magereza, Zimamoto na Jeshi la Akiba)	Mabadiliko ya tabia kwa Askari baada ya kupata elimu ya kuzuia rushwa, ushirikiano wa kupata taarifa za rushwa na kubadilishana uzoefu katika kazi.
5.	Mahakama	Kubadilishana uzoefu katika utendaji kazi, ushauri wa kitaalamu, elimu ya kuzuia rushwa kwa Watumishi wa Mahakama, kushirikiana katika maadhimisho mbalimbali kama Wiki ya Sheria n.k	Kuboresha utendaji kazi katika Taasisi hizi mbili, kuimarishwa kwa mahusiano kati ya Taasisi hizi.
6.	AZAKI na Sekta Binafsi.	Kushiriki katika utoaji elimu kwa wananchi, kushiriki matamasha na maonesho yanayoandaliwa na TAKUKURU, Kushirikiana katika Maadhimisho mbalimbali	Upatikanaji wa taarifa zinazohusu viashiria vya rushwa na kuongezeka kwa hamasa ya Wananchi katika kushiriki mapambano dhidi ya rushwa.

5. MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA

S.N	Shughuli iliyofanyika	Mdau tuliyeshirikiana nae
1.	Maonesho yaliyohusu kuelezea kazi za TAKUKURU na utoaji elimu ya mapambano dhidi ya rushwa.	Mahakama, Mawakili, Wanafunzi wa Sheria toka Vyuo vikuu vya Iringa, Wananchi, AZAKI, Wanaklabu za Wapinga Rushwa na Taasisi za Umma.
2.	Utoaji wa elimu katika Magereza, Vyuo vikuu vya Iringa na katika vituo vya redio.	Mahakama, Mawakili wa kujitegemea, Mawakili wa Serikali na Wahadhiri wa Vyo vikuu.

6. MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI.

S.N	Shughuli iliyofanyika	Mdau tuliyeshirikiana nae
1.	Utoaji wa elimu kwa wadau mbalimbali wanaotetea haki za Wanawake.	AZAKI, Taasisi mbalimbali za Serikali, Vyombo vya Ulinzi na Usalama ikiwamo na Polisi (Dawati la Jinsia).
2.	Kushiriki katika kazi za kusaidia jamii katika Kata mbalimbali.	Watumishi wa Serikali za Mitaa (Maendeleo ya Jamii), AZAKI na Wananchi (Kinamama)
3.	Kushiriki maadhimisho ya Siku ya Wanawake kiwilaya na kimkoa	AZAKI, Idara za Serikali za Mitaa na Vyombo vya

7. MIKAKATI YA APRILI HADI JUNI 2023

- TAKUKURU Mkoa wa Iringa, inatarajia katika robo ya **Aprili-Juni 2023,** kuimarisha juhudi za kuzuia rushwa kwa kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika kuzuia rushwa kupitia nyenzo mbalimbali za uelimishaji ikiwemo mikutano ya hadhara, vipindi vya redio pamoja na uimarishaji wa Klabu za Wapinga rushwa mashuleni.

- Kuendelea na utekelezaji wa Programu ya **TAKUKURU Rafiki** kwa Wananchi kwa lengo la kuongeza ushiriki wa Wananchi na Wadau katika kukabili tatizo la rushwa katika utoaji wa huduma kwa Jamii na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

- Kufanya Makongamano kuhusu Kukuza Maadili na Elimu kuhusu Vita Dhidi ya Rushwa katika Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu katika mkoa wa Iringa ili kuwajenga vijana katika Uzalendo na Uadilifu.

- Kufanya udhibiti wa mapato ya Serikali na usimamizi wa Rasilimali za Umma ikiwa ni pamoja na **udhibiti** wa fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kuchukua hatua stahiki kwa wale watakaobainika kufuja mali za Umma kwa kufanya chunguzi na kuwafikisha katika vyombo vya Sheria unapopatikana ushahidi wa kutosha.

- Kufanya uchambuzi wa mifumo na warsha na wadau kujadili matokeo ya chambuzi za mifumo zilizokamilika ili kuweka maazimio ya namna bora ya kuziba mianya ya ufujaji iliyobainishwa.

8. WITO KWA WAKAZI WA MKOA WA IRINGA

TAKUKURU Mkoa wa Iringa inatoa wito kwa Wananchi kuendelea kuunga mkono jitihada za Kufichua vitendo vya rushwa na wala rushwa, kwa kutoa taarifa sahihi zitakazowezesha kuwachukulia hatua wahusika.

Tunawasihi Watumishi wa Umma na Sekta binafsi watekeleze majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za kazi zao ili kuzuia vitendo vya rushwa na kuleta tija katika kuhudumia wananchi.

"KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU; TUTIMIZE WAJIBU WETU"

Imetolewa na:

Domina J. Mukama
MKUU WA TAKUKURU (M)
IRINGA
Simu: **0738150084**